Alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akitawadha kila wakati wa swala

Kutoka kwa Amri bin Aamiri kutoka kwa Anasi amesema: Alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akitawadha kila wakati wa swala, nikasema: Nyinyi mlikuwa mnafanya vipi? Akasema: Ulikuwa ukimtosha mmoja wetu udhu mmoja madam hajatengukwa.

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Alikuwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akitawadha kwa kila swala ya faradhi hata kama hajatengukwa udhu; Na hii ni kwa sababu ya kupata malipo na fadhila. Na inafaa kwa mtu kuswali kwa zaidi ya swala moja kwa udhu mmoja madam bado yuko na udhu wake.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/65080